

## **TARATIBU ZA KUZINGATIA KWA UVUVI WA KAMBAMITI KWA MSIMU WA MWAKA 2021.**

Uvubi wa Kambamiti kwa msimu wa mwaka 2021 utafanyika kwa kuzingatia Sheria ya Uvubi Namba 22 ya mwaka 2003, Kanuni za Uvubi za mwaka 2009 na maboresho yake ya mwaka 2020 pamoja na taratibu nyingine ambazo zimeandaliwa na Wizara. Taratibu hizo ni kama zifuatazo:

- i. Uvubi wa Kambamiti utafunguliwa tarehe 1 Machi mpaka tarehe 30 Septemba kwa Kanda ya Kaskazini na tarehe 1 Aprili mpaka tarehe 31 Agosti kwa Kanda ya Kusini kila mwaka kwa wavubi wote wakubwa na wadogo.
- ii. Kila muombaji atapaswa kujaza kikamilifu fomu (3b na QA/APP/10) wakati wa maombi kwa kuzingatia Sheria ya Uvubi Na. 22 ya Mwaka 2003 na Kanuni zake za Mwaka 2009 na Marekebisho yake ya mwaka 2020.
- iii. Maombi ya leseni za uvubi wa Kambamiti kwa wavubi wakubwa yatumwe kwa Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvubi (Uvubi) na wavubi wadogo watume maombi katika Halmashauri husika.
- iv. Kila chombo kitapata haki sawa. Aidha, utaratibu utakaotumika kuhusu chombo gani kinaanza mwezi machi na chombo gani kitaendelea mpaka mwezi septemba utapangwa na wadau watajulishwa.
- v. Kila Kampuni ya Meli iliyopata kibali cha kuomba leseni itapaswa kuwasilisha 'Bank Statement' inayoonyesha uhai wa biashara husika.
- vi. Makampuni yanashauriwa kuwekeza katika viwanda vya kuchakata mazao ya Uvubi, viwanda vya kutengeneza barafu kwa ajili ya kuhakikisha ubora wa mazao ya uvubi. Aidha, kwa wale ambao watakuwa wameshindwa kuwekeza katika viwanda, wanashauriwa kuwasilisha mikataba ambayo wameingia na wenye viwanda kwa ajili ya kuhifadhia na kuchakata mazao ya uvubi ili kuhakikisha ubora wa mazao unazingatiwa.
- vii. Kwa Makampuni yatakayoajiri wageni, yanapaswa kuwasilisha vibali vya kufanya kazi nchini kwa watu wasio raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- viii. Idadi ya meli kwa wavubi wakubwa zitakuwa kumi na mbili (12) ambapo kila kanda zitaruhusiwa meli nne tu ambapo kutakuwa na mzunguko kwa kanda kila mwezi.

- ix. Vyombo vitakavyotumika kwenye Uvuvi wa Kambamiti vitatakiwa kuwa na injini zisizozidi jumla ya nguvu ya Farasi 500 (500HP) na urefu kati ya mita 11.11 hadi mita 25.0, uzito usiopungua tani 20 na usiozidi tani 150 (GRT).
- x. Meli ya uvuvi hairuhusiwi kutumia mnyororo wa kutifua tifua chini (tickler chain) katika Uvuvi wa Kambamiti.
- xi. Wavu uwekewe kifaa kisichokamata viumbe adimu kama vile Kasa (Turtle Exclusive Device-TED) na kupunguza samaki wasiolengwa (Bycatch Reducing Device-BRD).
- xii. Meli inayokokota wavu nyuma (stern) iwe na wavu mmoja na meli inayokokota wavu ubavuni (outriggers) iwe na nyavu mbili (moja kila upande).
- xiii. Chombo cha uvuvi ni lazima kiwe na kifaa kitakachoonyesha mwenendo wa meli ya Uvuvi Baharini (VMS). Gharama za kuweka kifaa cha VMS kwenye meli iwe ni ya mwenye chombo. Aidha, VMs inapaswa kuwashwa muda wote wa chombo kiwapo baharini.
- xiv. Muda wa kuvua kwa meli utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili asubuhi mpaka saa kumi na mbili jioni.
- xv. Eneo la Uvuvi kwa meli zisivue chini ya kina cha mita 6 kulingana na mkataba wa RAMSAR.
- xvi. Chombo kitakachovua kiwe na 'Fishing Authorization Certificate' kutoka nchi ambayo meli hiyo ilikuwa inavua kwa mara ya mwisho.
- xvii. Chombo kiwe na usajili kutoka TASAC na kupewa Sea worthness certificate.
- xviii. Chombo kitakachoomba kuvua kitakaguliwa kama hakijahusika kwenye Uvuvi haramu.
- xix. Takwimu zitakazowasilishwa wakati wa kushusha mzigo zitathibitishwa na nahodha wa chombo na "Observer wa Idara" kwa kusainiwa na wote.
- xx. Utoaji wa leseni utazingatia 'Kampuni moja meli moja' ili kuhakikisha kuwa kila kampuni inamilikiwa na mmiliki tofauti.

- xxi. Ikiwa itabainika kwamba "Observer", Nahodha na "Chief Officer" wameshiriki katika kutorosha mzigo au kutoa taarifa zisizo sahihi hatua kali za kisheria zitachukuliwa.
- xxii. Idara ya Uvuvi itatoa kibali kwa meli kushusha samaki (bycatch) Bandarini au baharini. Aidha, chombo chochote hakiruhusiwi kumwaga samaki majini.
- xxiii. Chombo chochote hakiruhusiwi kuchafua mazingira kama vile kutupa takataka ngumu (Plastics), Mafuta na uchafuzi mwengine unaofanana na huo.
- xxiv. Meli zitakapokuwa zinavua kwenye kanda husika zifanye mawasiliano na Serikali ya Kijiji/Mtaa, mara watakapofika kwenye eneo lao na watoe taarifa wakati wanaondoka na kulipa ushuru stahiki.